

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS – TAMISEMI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI

Simu Namba. **0755 - 625224** Shule ya Sekondari Longoi,  
Barua pepe. [nelsonmilka@gmail.com](mailto:nelsonmilka@gmail.com) S. L. P 1009,  
Kumb Na. LSS/GA/V/21Moshi.  
**Tarehe. 15 – 01 – 2020.**



**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi .....**

S. L. P .....

.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2021 KATIKA  
SHULE YA SEKONDARI LONGOI IYOPO WILAYA YA HAI MKOA  
WA KILIMANJARO.**

**1.0 Utangulizi**

Ninafurahi kukutaarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha **KWANZA** katika shule hii mwaka **2021**. Shule ya Sekondari **LONGOI** ipo umbali wa km **22** kusini mwa Halmashauri ya **HAI**.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **11 – 01 – 2021**na mwanao anatakiwa kuripoti shulenii kuanzia tarehe **11 – 01 – 2021**na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18 – 01 – 2021**ndani ya siku saba.

**2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia**

**2.1 Sare za Shule**

**a) WAVULANA**

Suruali 2 za rangi ya **KIJANI (DARK GREEN)**, shati nyeupe 2 za mikono mifupi viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi na vya kamba, soksi nyeusi pea 2, – ona kitambaa kilichoambatishwa kwa ajili ya Suruali. Sweta liwe la rangi ya Suruali na shingo iwe ya **V**.

**Maelezo ya mshono;**

Suruali iwe ya marinda mawili (2), iwe na mifuko ya pembeni sio kama ya jinsi, iwe na mifuko mmoja wa nyuma wa kufunga kwa kifungo sio zipu, pia iwe ndefu na yenye pindo chini mwisho (**Turn up**), iwe na upana kuanzia **15cm**.

**b) WASICHANA**

Sketi 2za rangi ya **KIJANI – DARK GREEN** na shati nyeupe 2 za mikono mifupi, soksi nyeupe joz 2 zinazofika nusu ya mguu, viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi na vya kamba – ona kitambaa kilichoambatishwa kwa ajili ya Sketi. Sweta liwe la rangi ya Sketi na shingo iwe ya **V**.

**Maelezo ya mshono;**

Sketi iwe ya **Rinder box**, belti lisiwe kubwa liwe la kawaida na pia iwe ndefu urefu toka kwenye goti kwenda chini iwe **cm20**, kiuno kiwe na upana wa nchi **2½” (Usishone kantangaze)**.

**c) KWA WAISLAMU**

Msichana ashone “**short kanzu**” nyeupe ndefu. Rangi ya Hijab ifanane na Sare za shule (iwe nyeupe sawa na “**short kanzu**”. na iwe ndefu inayofunika mabega hadi mikono).

**PATA MAELEKEZO ZAIDI SHULENI.**

2.2. Sare ya michezo

**WAVULANA**

**Bukta nyeusi, T – sheti nyekundu**

**WASICHANA**

**Bukta nyeusi, T – sheti nyekundu**

2.3. Daftari, kalamu na mkebe wa hesabu.

2.4. Awe na begi la kubebbea daftari.

2.5. Aje na FAILI (file) kwaajili ya kutunza kumbukumbu zake za darasani.

**3.0 MAHITAJI MENGINE:**

(i) Kila mwanafunzi awe na Sahani na Kijiko kwa ajili ya chakula.

3.1 Vifaa vya usafi na kazi ndogondogo za nje ya darasa.

Mwanafunzi afikapo shulenii afike na kifaa kifuatacho:-

- i. Jembe lenye mpini moja(1)
- ii. Ndoo ndogo ya plastiki moja(1) na Ufagio wa chelewa mmoja (1)
- iii. Fyekeo moja (1)

**NB:**Mwanafunzi ataleta mojawapo ya vifaa tajwa hapo juu.

#### **4.0 Sheria na Kanuni Muhimu za Shule hii**

3.1 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundis, yenyе dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenyе jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shulen:-

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation);
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- g) Kuva sare ya shule wakati wote uwapo shulen;
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
- i) Kutunza mali za umma.

#### **3.2 Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Kufukuzwa au kusimamishwa Shule (Masomo)**

- a) Wizi.
- b) Uasherati na ushoga.
- c) Ubakaji.
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyaa kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi n.k.
- e) Kupigana au kupiga.
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- g) Kudharau Bendera ya Taifa.
- h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba.
- i) Kuoa au kuolewa.
- j) Kutoa mimba.
- k) Kugoma, kuchochea na kuongoza, kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- m) Kuwa na simu ya mkononi.
- n) Utoro.

#### **4.0 Mambo Mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shulen na mwanafunzi**

- a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkoo wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkoo wa Shule mara utakaporipoti shulenii.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
- d) Tafadhalii soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**NB:** Hakikisha kuwa unamleta mwanaao shulenii na kumkabidhi mara tu shule itakapofunguliwa.

Endapo mwanafunzi/mzazi/mlezi atakuwa na dharura awasiliiane kwa kutumia simu ya shule.

Mwisho natumia fursa hii kwa niaba ya walimu, wafanyakazi na wanafunzi wote wa shule hii kukukaribisha hapa shulenii na naamini utatumia vizuri nafasi hii uliyopewa na Taifa.

### KARIBU SANA LONGOI SEKONDARI



MILKA N. MREMA

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE  
LONGOI SEKONDARI  
S. L. P. 1009 MOSHI

Jina la Mwanafunzi .....

S. L. P .....

Tarehe .....

MKUU WA SHULE,

SHULE YA SEKONDARI LONGOI,

S. L. P 1009,

MOSHI.

**YAH: UCHAGUZI WA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA .....**

1. Asante sana kwa barua yako yenye Kumb.Na. LSS/G/J/Vol. ....../..... ya tarehe ...../...../20..... ya kunijulisha kuwa nimechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza shulenii hapo.
2. Ninatoa ahadi kutii sheria zote za shule ambazo nimezisoma na kuzielewa.
3. Ninakubali/ sikubali nafasi hii niliyopewa na Taifa.
4. Niko tayari kutimiza maagizo yote niliyopewa kujiunga na shule hii.
5. Historia fupi ya Mwanafunzi husika.

PICHA YA  
MWANAFUNZI

Jina kamili uliloandikishwa shulenii	Shule ya Msingi na Sekondari ulizopitia	Tarehe ya kuzaliwa	Mahali unapoishi/ulipozaliwa Kijiji/Kitongoji/Mtaa	Dini/Dhehebu	Uraia
	MSINGI		Kijiji		
	SEKONDARI		Kitongoji/Mtaa		

Nakiri kuwa maelezo yote niliyotoa hapo juu ni sahihi.

6. Jina kamili la Mwanafunzi ..... sahihi ..... tarehe .....
7. Sehemu ya Mzazi/Mlezi kukubali kuchaguliwa kwa mwanafunzi/mtoto husika.

PICHA YA  
MZAZI/MLEZI

7.1 Jina la Mzazi/Mlezi ..... Kazi .....

7.2 Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi .....

7.3 Anuani ya Mzazi/Mlezi .....

7.4 Mahali anakoishi:

Kijiji ..... Kitongoji/Mtaa .....

**Tamko la Mzazi/Mlezi**

Ninakiri kuwa mimi ni Mzazi/Mlezi wa

.....Ninakubali/sikubali nafasi hii aliyopewa mwanangu ya kujiunga na shule hii. Nakubali/sikubali sheria na maagizo yote ya shule aliyopewa ya kujiunga na shule hii. Naahidi kumhudumia mwanangu na uongozi wa shule kufanikisha elimu yake.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi ..... Tarehe .....

**\*FUTA ISIYOHITAJIKA\***

PRESIDENT'S OFFICE– RALG  
HAI DISTRICT COUNCIL  
LONGOI SECONDARY SCHOOL

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

Name of Student .....

To Medical Officer,

District/Regional/Designated Hospital

Please examine the above named student in full as to his/her physical and mental fitness for being able to pursue Ordinary Secondary School Education for four years.

1. Eye sight. ....
2. Hearing.....
3. Speech. ....
4. Heart examination. ....
5. Blood pressure. ....
6. STDs & STPs. ....
7. Epilepsy. ....
8. Asthma. ....
9. TB. ....
10. Diabetes. ....
11. Sickle cell. ....
12. Tropical ulcer. ....
13. Tumours (breasts). ....
14. Pregnancy test (for Girls). ....
15. Neurosis. ....
16. Other observations  
.....  
.....

I have examined the above named student and consider him/her physically and mentally fitness to pursue with Ordinary Secondary School Education.

NAME. ....

SIGNATURE. .... DATE. ....

DESIGNATION .....

STATION. ....

OFFICIAL STAMP.....